# JINSI YA KUTAYARISHA CHOMBO KINACHOINAMISHWA KWA AJILI YA KUNAWA MIKONO UKITUMIA KIASI KIDOGO CHA MAJI

**Kadi ya Nasaha**

## Vitu Unavyovihitaji:

1. Matawi mawili ya mti (yenye urefu wa mita 2, na yenye umbo la Y mwishoni)
2. Vijiti viwili vyembamba vyenye urefu wa mita 1 (kimoja cha kuangikia mkono wa chombo, na kingine cha kusukuma kwa mguu)
3. Msumeno wa kukatia vijiti
4. Msumari wenye urefu wa sentimita kati ya 8 na 11
5. Kitambaa au koleo
6. Mahali penye moto (ulimi wa moto)





7. Sepetu au beleshi
8. Vipande viwili vya kamba (kimoja chenye urefu wa nusu mita (0.5m) cha kuweka katika kifuniko; kingine cha mita1cha kufungia katika kijiti cha kusukuma kwa mguu
9. Kibuyu yenye ujazo wa lita 3 au 5
10. Sabuni
11. Kipande cha mti chenye urefu sawa na urefu wa kipande cha sabuni
12. Bisibisi au kifaa cha kutobolea tundu katika sabuni
13. Mawe, changarawe za kuweka katika shimo

## Jinsi ya Kutayarisha chombo kinachoinamishwa kwa ajili ya kunawa mikono:

**1** **Weka alama katika sehemu ambapo utatoboa tundu.** Tafuta chombo kitupu cha plastiki chenye ujazo wa lita 3 au 5. Weka alama pale ambapo utatoboa tundu, kama sentimita 2 hivi chini ya kifuniko.



**2** **Pasha msumari moto.** Shika msumari ukitumia koleo au kitambaa na upashe msumari moto ukitumia ulimi wowote wa moto.



**3** **Toboa matundu.** Ukitumia msumari wenye moto, toboa tundu katika chombo na tundu lingine katika kifuniko.





**4** **Weka kamba.** Weka sehemu ndefu ya kamba (mita 1) kupitia tundu ulilotoboa katika kifuniko. Anza kwa kuvuta sehemu ya mwisho ya kamba kupitia upande wa nje wa kifuniko ili kipande cha kamba kisichofungwa kiwe ndani ya kifuniko.



**5** **Piga fundo katika kamba.** Piga fundo katika kipande cha kamba kilicho ndani ya kifuniko. Piga fundo lililo kubwa vya kutosha kiasi kwamba fundo haliwezi kuvutwa likapita katika tundu. Weka kifuniko katika chombo na ukaze kwa kuzungusha. Fundo sasa linakuwa ndani ya chombo na ile sehemu ndefu ya kamba iliyoachwa huru inakuwa nje ya chombo.



**6** **Unganisha na kijiti (cha kusukuma kwa mguu).** Funga sehemu ya kamba iliyobaki katika kijiti cha mita 1. Baada ya hayo, kijiti kitakuwa kimeunganishwa na chombo kwa kamba. Hiki ndicho kijiti cha kusukuma kwa mguu kinachotumiwa katika chombo kinachoinamishwa wakati wa kunawa mikono.

*Kumbuka—Unaweza kubadilishsa urefu wa kamba, ukitaka, katika hatua ya 11.*



Instructions adapted from, "How to Make a Tippy Tap – A hygienic handwashing device with running water. Authors/Photos Mark Tiele Westra. Werkgroep OntwikkelingsTechnieken (WOT); University of Twente, the Netherlands; Henk Holtslag Connect International.

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE | HIP HYGIENE IMPROVEMENT PROJECT

THE REPUBLIC OF UGANDA
Ministry of Health

Plan
Be a part of it.

**7** **Toboa tundu katika sabuni.** Tumia kifaa (k.m. bisibisi, kijiti) kutoboa tundu katika sabuni kwa kuzungusha na kusukuma kifaa hadi kipitie katika sabuni.



**8** **Ingiza kamba.** Sukuma kipande kile kingine cha kamba kilicho kifupi (nusu mita) kupitia katika tundu ulilotoboa katika sabuni, kisha uunganishe kamba na kijiti kifupi au kipande cha ubao.



**9** **Jaza chombo.** Jaza chombo na maji hadi kiwango cha tundu.



**10** **Weka nguzo ardhini.** Amua wapi bora pa kuweka chombo kinachoinamishwa wakati wa kunawa mikono. Iweke sehemu ambapo watu huenda kunawa mikono mara kwa mara (karibu na choo au jiko). Ukitumia sepetu/beleshi, tengeneza mashimo mawili ya kina cha sentimita 50 ardhini. Zitenganishe nguzo kwa sentimita 70. Ziweke nguzo katika mashimo, uweke udongo na kuugandamiza.



**11** **Angika kibuyu, kijiti cha kusukuma kwa mguu, na kamba yenye sabuni.**

- Pitisha kijiti katika mkono wa kibuyu na uweke kijiti hicho kati ya nguzo mbili. Baada ya kufanya haya, kibuyu sasa iwe inaning'inia katika kijiti.
- Ifunge kamba yenye sabuni karibu na kibuyu ili iwe inaning'inia katika kijiti. (Kama hakuna sabuni, tumia chombo cha kuwekea majivu).
- Hakikisha kuwa kamba ya kijiti cha kusukuma kwa mguu ili maji yaanze kutiririka imewekwa kwa njia ambayo sehemu moja ya kijiti imeinuliwa kiasi cha sentimita 15 juu ya ardhi, na sehemu nyingine inalala chini ardhini.



**12** Tengeneza shimo. Tengeneza shimo (lenye urefu wa sentimita 40 x 40 na kina cha sentimita 20) chini ya kibuyu ambapo maji yatamwagika). Jaza shimo hilo na mawe makubwa. Hili ndilo shimo la mawe ambalo linazuia sehemu hiyo yenye chombo kinachoinamishwa isiwe na matope, na tena kuwa eneo linalotumiwa na mbu kuzaa.



## Ili Kutumia:

Sukuma kijiti chini kwa mguu. Hii itakifanya chombo kiiname na kuyafanya maji yatoke kupitia tundu. Mwaga maji katika mikono kisha uachie kijiti. Shika sabuni au majivu) na usugue. Sukuma kijiti chini tena na usuuze mikono.



## Jinsi ya Kutunza Chombo Kinachoinamishwa kwa ajili ya Kunawa Mikono:

1. Hakikisha kuwa chombo chako kina maji wakati wote kwa kukijaza tena ili kiwe tayari kutumiwa wakati wote.
2. Osha chombo nje na ndani kila wiki au kabla kama kikionekana kuwa kichafu.
3. Sabuni (au majivu) ikiisha, tia sabuni (au majivu) nyingine.
4. Weka vijiti vingine baada ya muda na usiache vile ulivyoweka kwanza, kuvunjika.